HOTUBA YA WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MHESHIMIWA KASSIM MAJALIWA MAJALIWA (MB) WAKATI AKIFUNGUA MAFUNZO KWA WAKUU WA MIKOA NA MAKATIBU TAWALA WA MIKOA TAREHE 03 DESEMBA, 2018 – JIJINI DODOMA

- **Mheshimiwa Selemani Jafo (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI),**
- **Mheshimiwa Kapt. (Mst.) George Mkuchika (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora,**
- **Balozi Mhandisi John Kijazi, Katibu Mkuu Kiongozi,**
- **Mhandisi Mussa Iyombe, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais – TAMISEMI,**
- **Mhe Dr. Binilith Mahenge, Mkuu wa Mkoa Dodoma,**
- **Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa,**
- **Makatibu Tawala wa Mikoa,**
- **Wakurugenzi wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI,**
- **Watendaji wa Taasisi ya UONGOZI**
- **Wawezeshaji wa Mafunzo,**
- **Wanahabari,**
- **Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana.**

1. UTANGULIZI

Awali ya yote napenda kuwakaribisha katika jiji la Dodoma, karibuni sana. Kama mnavyofahamu tarehe 5/9/2018, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilipitisha Sheria ya kulitangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu rasmi ya Nchi kisheria. Kwahiyo, tangu tarehe 24/9/2018 Sheria hiyo ya "The Dodoma Capital City Declaration Act 2018, iliposainiwa na Mheshimiwa Rais; Jiji la Dodoma ni Makao Makuu Rasmi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivyo, karibuni sana Makao Makuu ya Nchi. Nafurahi kwamba Mwenyeji wetu Mheshimiwa Dkt. Binilith Mahenge; ambaye eneo lake la Utawala kwa sasa ndiyo Makao Makuu; ni miongoni mwa viongozi washiriki katika mafunzo haya.

Kabla sijaendelea napenda kutumia fursa hii kuwasilisha kwenu salamu kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mheshimiwa Samia Hassan Suluhu, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wote kwa pamoja wanawapongeza kwa majukumu na wanawasalimu sana.

Napenda pia nitumie fursa hii kuwashukuru waandaji wa mafunzo haya ambayo amenipa heshima ya kuyafungua. Ninawashukuru wote waliofanikisha kuandaliwa kwa mafunzo haya, yaani Ofisi ya Rais – TAMISEMI, wawezeshaji, ambao wao binafsi wamekubali kuja kutoa mada na ufafanuzi kwa maeneo yatakayohitaji ufafanuzi. Nawashukuru pia Taasisi ya UONGOZI ambayo Dira na Dhima yake ni kuwaimarisha Viongozi wa Afrika ikiwemo Tanzania, ili matokeo ya Uongozi wao yawapatie matokeo endelevu wananchi dhidi ya changamoto mbalimbali zinazowakabili kwenye maeneo yao.

Ni dhahiri kuwa tangu Taasisi ya UONGOZI ianzishwe; imetoa mchango mkubwa katika mafanikio ya Serikali kwa kutoa mafunzo kwa viongozi wa ngazi mbalimbali.

Ndugu Viongozi,

Kumbukeni kuwa ninyi ni viongozi tegemeo katika utekelezaji wa Sera za Serikali. Mnayo dhamana ya kumsaidia Mhe. Rais kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015; pamoja na maelekezo yake mengine ambayo Rais huyatoa kwa mujibu wa Katiba. Kwa muktadha huo; katika hotuba yangu nitawakumbusheni pia kuhusu wajibu wa kila mmoja wetu hususan, ushirikiano unaohitajika kwenye utekelezaji wa kazi za kila siku; ambazo takribani zote zinalenga kumhudumia vizuri Mtanzania.

LENGO LA MAFUNZO

Ndugu Viongozi,

Napenda kuwajulisha kuwa Mheshimiwa Rais na sisi wasaidizi wake tuna imani kubwa na uongozi na utendaji wenu; hatuna shaka yoyote maana mlipekuliwa sana wakati wa mchakato kuelekea uteuzi wenu. Ninawapongeza kwa uongozi na utendaji kazi wenu mzuri mliouonesha tangu mlipokabidhiwa Ofisi hadi sasa. Kwa waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, wasimamizi wakuu wa shughuli zote za Serikali katika Mikoa yenu, na Makatibu Tawala wa Mikoa, mkiwa Watendaji Wakuu na Maafisa Masuuli katika Mikoa yenu; huu ni wakati mzuri kuijimarisha zaidi katika Uongozi na Utendaji. Ni imani yangu kuwa baada ya semina hii mtakuwa viongozi na watendaji wazuri zaidi.

2. MADA ZITAKAZOWASILISHWA

Ndugu Viongozi,

Mada zote zilizochaguliwa ni muhimu na muafaka katika kuboresha Uongozi na Utendaji wenu. Ninawapongeza waandaji kwa kuchagua mada nzuri na muafaka. Kwa mfano;

(i) Kwenye mada inayohusu **Majukumu na Mipaka ya Kazi**; mtajifunza namna ya kufanya kazi bila mikwaruzano isiyo na tija baina yenu na viongozi wa mihimili mingine ya dola, viongozi wa kisiasa na watendaji wengine Serikalini

(Hasa nikitaja Majaji, Viongozi wa Chama Tawala, Wabunge, Mameya, Wenyeviti wa Halmashauri, Madiwani n.k.).

(ii) Kwenye mada inayohusu **Uongozi, Hisia na Mahusiano Mahali pa Kazi**; mtapata fursa ya kujiimarisha katika mbinu za kuwaongoza watumishi walio chini yenu kwa kujenga na kudumisha mshikamano na ushirikiano wa pamoja (*teamwork*). Mada itafafanua pia namna mnavyotegemeana na watumishi wa Kada na ngazi mbalimbali katika kutimiza majukumu yenu. Ni muhimu sana kufanya kazi kama timu moja ili muweze kuyafikia malengo ya Taasisi kwa upana wake na si malengo ya mtu/kiongozi mmoja.

(iii) Kwenye mada inayohusu **Muundo wa Serikali na Namna Serikali inavyofanya Kazi**; mtauelewa vizuri zaidi Muundo wa Serikali ulivyo na jinsi unavyofanya kazi. Mtaielewa vizuri zaidi itifaki na kuheshimiana kwa ngazi mbalimbali kutoka Waziri, Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, Makatibu Tawala, Wakurugenzi, Wakuu wa Idara hadi Wananchi. Masuala kuhusu mwenendo unaotakiwa, tabia, mavazi, mazungumzo, uhusiano wa kikazi, matumizi ya simu na mitandao ya kijamii n.k., yatagusiwa pia. Sikilizeni kwa makini sana ili mjiimarishe vizuri zaidi kwenye eneo hili.

(iv) **Utunzaji wa Siri za Serikali** ni mada nyingine itakayowasilishwa. Katika mada hii mtaielewa vizuri zaidi dhana ya siri; nafasi ya siri katika uendeshaji wa Serikali; na wajibu wenu katika kuthibiti uvujaji wa siri za Serikali katika kipindi hiki cha utandawazi wa mitandao ya kijamii. Naamini kila mmoja wenu atakuwa makini sana kwenye mada hii, kwani siri ndio uhai wa Serikali. Kwa kawaida mada hii inapowasilishwa hamtaruhusiwa kuandika wala kupatiwa vitini, hivyo, mtatakiwa kusikiliza kwa umakini mkubwa.

(v) Mtapatiwa pia mada kuhusu mambo mtambuka **mfano dawa za kulevya**, ambapo mtajadili na kubadilishana uzoefu kuhusu nafasi yenu kwenye

mapambano hayo na mbinu bora za mapambano kwenye medali hiyo ya vita ili kuiokoa jamii yetu dhidi ya athari za matumizi yake.

(vi) **Mawasiliano ya Kimkakati** ni mojawapo ya mada ambayo itatolewa katika mafunzo haya, katika mada hiyo, mtaelezwa namna bora ya kufanya mawasiliano hayo kama viongozi. Lini, wakati gani na namna gani ya kufanya mawasiliano hayo mtajulishwa. Hii itawasaidia mawasiliano mnayofanya kwa umma yawe ni yenye tija na muweze kuelezea kwa ufasaha masuala makubwa yanayofanywa na serikali katika Mikoa yenu.

(vii) **Viashiria Hatarishi na Usimamizi wa Ndani, Masuala ya Manunuzi katika Sekta ya Umma** ni moja ya mada zitakazowasilishwa katika mafunzo haya. Hapa mtafahamu viashiria hatarishi na namna ya kuvizuia lakini pia mtafahamu kwa muhtasari taratibu za manunuzi katika Sekta ya Umma, hii itawasaidia kusimamia thamani ya fedha katika miradi inayoendelea katika maeneo yenu.

Kupitia mada hizo; mtapata fursa ya kutafakari na kujithamini kuhusu hatua za kujiimarisha zaidi kiuongozi na kiutendaji. Hatua hizo ni lazima ziwe pamoja na kubadilika kwa mtazamo na kujirekebisha endapo mtabaini maeneo mliyokuwa mkikosea tangu mlipokabidhiwa Ofisi hadi sasa.

3. MATARAJIO BAADA YA MAFUNZO

Ndugu Viongozi,

Mada zote hizo zina maudhui mahsusi, na zina lengo la kuboresha eneo mahsusi. Hivyo, baada ya mafunzo haya, natarajia kuwa;

(i) Mtasimamia kikamilifu nidhamu katika Utumishi wa Umma na ninyi wenyewe mtakuwa kioo katika kuzingatia miiko ya Utumishi wa Umma;

(ii) Mtazingatia kikamilifu mipaka yenu ya madaraka na kwamba hatua mtakazozichukua katika Uongozi na Utendaji wenu zitazingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo;

(iii) Mtasimamia kikamilifu mapambano dhidi ya madawa ya kulevya;

(iv) Mtadhibiti uvujaji wa Siri za Serikali katika zama hizi za utandawazi na mtakuwa mstari wa mbele katika kutunza Siri za Serikali. Watumieni vizuri wataalamu wa Usalama ikiwa ni pamoja na wataalamu wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kukabiliana na uvujaji wa siri kupitia mitandao ya intaneti. Ikibidi kuwasiliana na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa masuala yanayohusu vidhibiti na ushahidi, fuateni utaratibu wa kuwasiliana nao.

(v) Mtadumisha uhusiano mwema baina yenu na watumishi walio chini yenu, kwa kuzingatia kuwa kila mtumishi anao mchango katika kuboresha utendaji kwenye kituo chake cha kazi. Nina matarajio makubwa kuwa mtadumisha uhusiano mzuri kikazi na viongozi wa juu na pia uhusiano wa diplomasia ya heshima na viongozi wengine ndani ya mihimili mitatu.

(vi) Mtafanya mawasiliano ambayo ni ya kimkakati zaidi yatakayojikita katika kuelezea mafanikio yaliyofanywa na Serikali na hayataleta migogoro katika jamii.

4. MAELEKEZO MAHSUSI

Ndugu Viongozi,

Pamoja na kwamba siku hii ni kwa ajili ya ufunguzi wa mafunzo; napenda kusisitiza masuala yafuatayo muyasimamie mtakaporudi kwenye vituo vyenu vya kazi;

- **Mpango Kazi**
  Hakikisheni kila mmoja wenu anaandaa mpango kazi unaoainisha shughuli zake za kila siku. Mkuu wa Mkoa, Katibu Tawala wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi na Wakuu wa Idara wote na Watumishi wote wawe na mpango kazi wa utekelezaji wa majukumu yao.

- **Uwajibikaji na Kutenda Haki**
  Simamieni nidhamu kazini na uwajibikaji wa Watumishi kwa wananchi. Aidha, nawasihi tendeni haki kwa wananchi na watumishi walio chini yenu (ni lazima watumishi wa Serikali wawapokee na kuwahudumia wananchi kwa staha, wawasikilize kero zao na kuzitafutia ufumbuzi);

- **Amani na Utulivu**
  Endeleeni kusimamia amani na utulivu kwenye Mikoa yenu ili watu waendelee kufanya shughuli zao bila wasiwasi wowote. Amani na Utulivu ndiyi itatuwezesha kama nchi, kuendelea kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuwekeza mitaji yao hapa nchini. Tunakumbushwa sisi viongozi tuhakikishe tunaziendeleza rasilimali za nchi hii kwa faida ya Watanzania wote bila kubagua jinsia, kabila, dini, rangi ya ngozi, mtu atokako ndani ya nchi ilimradi hajavunja sharia; wala ubaguzi mwingine wa aina yoyote. Tunaaswa tuwahudumie Watanzania wote kwa usawa;

- **Ufanyikaji wa Mikutano na Vikao vya Kisheria**
  Kasimamieni ili kila Mwenyekiti wa Kitongoji na Kijiji kwa Utaratibu wa Afisa Mtendaji wa Kijiji watimize wajibu wao wa kuitisha mikutano ya kisheria inayohusu mipango ya maendeleo pamoja na kuwapatia mrejesho wananchi kwa kuwasomea taarifa za mapato na matumizi. Fedha za ujenzi wa miundombinu mbalimbali kama madarasa, vyoo, nyumba za walimu, zahanati na kadhalika; lazima kwenye mikutano hiyo, wananchi wapewe mrejesho kwa usahihi. Kutokuwa na mrejesho wenye ukweli na uwazi kuhusu michango

wanayochangishwa na utekelezaji kwa ujumla wa miradi ya Maendeleo kwenye vijiji vyao hutoa nafasi ya wasiwasi wa wizi na ubadhilifu na kupunguza ari ya kujitolea. Waheshimiwa Madiwani nao ni lazima waongeze vikao vya kamati za Maendeleo za Kata kabla hawajahudhuria vikao vya mabaraza.

- **Migogoro ya Makundi Mbalimbali**
  Tumieni busara zenu katika kusuluhisha Migogoro iliyopo katika maeneo yenu kati ya Wakulima na Wafugaji kwa wakati na kwa kuzingatia Sheria za Nchi; Kanuni na Taratibu. Simamieni isiibuke migogoro mipya ya wakulima na wafugaji;

- **Migogoro ya Ardhi Nchini**
  Migogoro mingi imekuwa ikijitokeza katika maeneo yafuatayo:
  (i) Malalamiko ya kutolipwa fidia au kucheleweshwa;

  (ii) Malalamiko ya viwanja kumilikishwa kwa mmiliki zaidi ya mmoja;

  (iii) Wananchi kulipia kwa ajili ya kupimiwa viwanja lakini viwanja hivyo havikupimwa;

  (iv) Migogoro kati ya wananchi na serikali za vijiji/kata;

  (v) Migogoro kati ya Taasisi na wananchi;

  (vi) Migogoro baina ya wananchi kwa wananchi;

  (vii) Migogoro baina ya wamiliki wa migodi na wachimbaji wadogo wadogo wa madini.

Kwa kuwa migogoro ya ardhi imeendelea kuwa mingi katika maeneo yetu, hivyo nawaagiza kufiatilia kwa undani migogoro yote hiyo katika mikoa/wilaya zenu ili muweze kuweka mipango ya kuitatua na kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wake.

- **Usimamizi wa Miradi ya Maendeleo**
  Kasimamieni kazi na miradi inayowapunguzia umaskini Watanzania na kuwaletea maendeleo. Sekta za kilimo, mifugo, uvuvi, umeme, barabara, maji, elimu, afya, maliasili, utalii, madini na nyinginezo ni muhimu sana na tegemezi katika uboreshaji wa hali za maisha ya Watanzania.

- **Usimamizi wa Ushirika**
  Kasimamieni Ushirika ili kila mkulima apate malipo sahihi ya jasho lake; fuatilieni na zilindeni mali za wanaushirika zisifujwe; na washughulikieni wezi na wabadhilifu wa mali za wanaushirika kikamilifu ili tabia za zisiendelee kuwatia umaskini wanaushirika.

- **Ufanisi na Tija**
  Kasimamieni tija ya utendaji (performance). Miongoni mwa vigezo tunavyovitumia kupima tija ya utendaji kwenye halmashauri ni uwezo wa kukamilisha kazi ndani ya muda uliopangwa hasa kwa miradi ambayo huletewa fdha kamili kabla haijaanza. Mifano miradi ya vituo vipya vya afya. Unakuta Halmashauri A na B zinafanana hali ya hewa, upatikanaji wa vifaa, wataalamu, mafundi, hali za wananchi na kadhalika! Lakini Halmashauri A anakamilisha ujenzi wa kituo cha afya ndani ya miezi mine na fedha ikibaki; na anaitumia kukarabati majengo ya zamani; lakini Halmashauri B miezi 12 kituo hakijakamilika na fedha imeisha! Huo ni uzembe au kukosa uadilifu na uaminifu. Hakikisheni kila mtu anawajibika mahali pake pa kazi. Simamieni kwa nguvu zote mnayo madaraka makubwa. **YATUMIENI madaraka yenu vizuri** kuwasaidia Watanzania wapate huduma zilizokusudiwa na Serikali.

- **Matumizi ya Rasilimali za Umma**

  Napenda kuwakumbusha kuwa mnao wajibu wa kushughulikia watendaji wazembe na wabadhilifu kwenye Halmashauri zenu, viongozi msilee wizi na ubadhilifu kwenye maeneo yenu. Kila kiongozi lazima awe makini muda wote. Lazima kamati za Ulinzi na Usalama ambazo TAKUKURU ni wajumbe zifanye kazi ya ufatiliaji wa miradi yote ya maendeleo ili kusiwe na fedha zinazoibiwa kizembe au kutumika vibaya. Ubadhilifu unatakiwa kushughulikiwa mapema kwa weledi na utaalamu bila kulazimika kusimamisha utekelezaji wa miradi kwa muda mrefu. Lazima watu wachache ambao wamezoea kupanga njama za kuiba au kutumia vibaya fedha za umma washughulikiwe kisheria kama upo ushahidi wa wazi kabla hata CAG hajakagua. Lazima mianya yote ya ubadhilifu izibwe. Na zinapofunguliwa kesi dhidi yao lazima wanasheria wetu wahakikishe ushahidi kwa Serikali ili kutoa fundisho kwa wengine.

- **Udhibiti wa Madeni ya Watumishi**

  Kwa pamoja isaidieni Serikali kudhibiti madeni ya watumishi, ambayo wakati mwingine yanazalishwa kutokana na kuingia mikataba bila kuwepo uhakika wa fedha, uhamisho na stahili mbalimbali bila kwanza kutenga bajeti yake. Vile vile, hakikisheni malipo hewa, watumishi hewa, safari hewa na mambo mengine yanayofanana na hayo hayatokei kwenye maeneo yenu kwa kuyawekea mifumo ya kuidhibiti.

- **Ulinzi wa Wanafunzi wa Kike na Mahudhurio Shuleni**

  Waheshimiwa Viongozi, lisaidieni Taifa kukomesha tabia zinazorudisha nyuma maendeleo ya watu wetu ikiwemo kuwashughulikia vinara wa kupachika mimba wanafunzi. Ni aibu kubwa kwa Wilaya kuwa na idadi ya mimba za wanafunzi 100 au zaidi kwa mwaka wakati Kamati ya Ulinzi na Usalama ipo na eti ikisemekana wahusika walikimbia au wamefichwa! Watu wengine wanaendeleaa kuozesha wanafunzi. Yasimamieni masuala hayo yasiendelee kulitia aibu Taifa na pia dhibitini aina yoyote ya utoro. Hakuna sababu ya utoro hasa baada ya Rais wetu

Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kugharamia Shilingi 23.8 bilioni kila mwezi za elimu msingi bila malipo kuanzia elimu ya awali hadi kidato cha nne. Mzazi anagharamia mahitaji madogo madogo tu kama sare, madaftari, kalamu n.k. ambazo ziko ndani ya uwezo wao. Utoro ni kosa la jinai na mzazi kutompeleka shule motto nalo ni kosa la jinai. Kutelekeza watoto bila kuwahudumia nalo ni kosa la jinai kama ilivyo kuzurura na kuombaomba mitaani. Sheria Kuu ya Kanuni za Adhabu Sura ya 16 vifungu vya 166, 167, 169 A na 176 (b) vinadhibiti vitendo hivyo vyote itumieni.

- **Upatikanaji wa Huduma za Kijamii**
  Toeni kipaumbele katika kufuatilia na kusimamia sekta za afya, kilimo, elimu na maji, ambazo zinagusa zaidi maisha ya wananchi walio wengi. Aidha, fuatilieni na kuziba mianya yote ya upotevu wa dawa katika vituo vya kutolea huduma za afya pamoja na kusimamia ujenzi na ukarabati wa vituo vya afya unaoendelea katika maeneo yenu. Makatibu Tawala wa Mikoa mnapaswa kuwajulisha Wakuu wa Mikoa yenu kila fungu la fedha linaloletwa kwenye Halmashauri za Mikoa yenukutoka Serikalini au kwa wadau wengine; na kuwajulisha kuhusu hali na mwenendo wa ukusanyaji wa mapato na matumizi ya fedha za Halmashauri ili wasimamie na kuchukua hatua stahiki mapema.

- **Utekelezaji wa Miradi Kuzingatia Thamani ya Fedha**
  Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, mnalo jukumu kubwa la kufuatilia kwa karibu miradi ya maendeleo kwenye Mikoa yenu. Ni lazima muwe na taarifa sahihi kuhusu miradi ya maendeleo inayotelekezwa ili kuhakikisha kuwa miradi hiyo inalingana na thamani ya fedha iliyotumika na kama miradi hiyo inatimiza malengo yake ya kuwahudumia wananchi. Hatutaki kuendelea kuzalisha miradi kama ya baadhi ya masoko ya TASAF ambayo yalijengwa kwa fedha nyingi lakini hayatumiki kwa malengo yaliyokusudiwa. Ni lazima miradi iwe shirikishi ili iwafaidishe wananchi.

- **Maagizo Mbalimbali ya Viongozi Wakuu**
  Pokeeni na tekelezi maelekezo na maagizo ya viongozi wa juu na hakikisheni mnaandaa taarifa za utekelezaji wa maelekezo na maagizo hayo.

5. HITIMISHO

Ndugu Viongozi,

Mada zitakazowasilishwa siyo ngeni kwenu, lakini elimu ni bahari na haina mwisho. Sikilizeni, ulizeni maswali, jadilianeni kwa uwazi na msisite kuleta mapendekezo yenu Serikalini endapo yapo masuala mahsusi ya Kisera au Kisheria ambayo mnadhani yakirekebishwa, uongozi na utendaji wenu utaimarika zaidi.

Kuhusu hoja za Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG), jadilini kuhusu mfumo madhubuti utakaosaidia kumaliza hoja za CAG ambazo zimekuwa zikijirudia mara kwa mara. Serikali inapenda kumaliza au kupunguza kwa kiasi kikubwa hoja za CAG. Nimeambiwa Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali atatoa mada katika mafunzo haya, tumieni fursa hiyo kufahamu namna bora ya kudhibiti hoja zinazoongezeka kila mwaka. Endapo mtasimamia vizuri utendaji wa wahasibu, wahandisi, wataalamu wa ununuzi, maafisa mipango na wanasheria mnaweza kwa kiasi kikubwa kupunguza hoja za CAG.

Ndugu Viongozi,

Napenda kutumia fursa hii kumsisitizia kila mmoja wetu azingatie maadili na nidhamu katika maeneo ya kazi. Hakikisheni mnajitunza na kuwa picha nzuri ya mfano kwa wengine. Zingatieni sana **kuongoza na kutenda kwa njia shirikishi**. Ni lazima wakati wote, mtafute njia bora ya kuwashirikisha wengine ili msingi wa uongozi na utendaji wenu uegemee zaidi kuleta maendeleo kwa wananchi.

Mwisho kabisa, ninawashukuru wote kwa kufika kwenye mafunzo haya muhimu. Hata hivyo, kabla ya kumaliza hotuba yangu nielekeze kuwa, hakikisheni mnashiriki

kikamilifu katika mafunzo haya, sitarajii ushiriki hafifu kutoka kwenu, hii itaondoa lengo zuri la umuhimu wa mafunzo haya, tulieni katika nyumba ya mafunzo, wasikilizeni wakufunzi wakati wa uwasilishaji wa mada na wakati wa majadiliano. Kumbukeni kuwa Mheshimiwa Rais ameridhia mafunzo haya yafanyike baada ya kumwelezea umuhimu wake. Hivyo, ni matarajio yake mtayapa mafunzo haya umuhimu unaotakiwa na kuwarahisishia kazi wakufunzi wa mafunzo haya. Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI simamia hilo, hakikisha viongozi hawa wanashiriki kikamilifu bila kuanza kutoa udhuru usio na tija na katika hili nitahitaji unipe mrejesho wa ushiriki wa kila mmoja wao.

Baada ya maelezo haya, napenda sasa kutamka kuwa mafunzo haya ya Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wa Mikoa yamefunguliwa rasmi.

Ahsanteni kwa kunisikiliza!